**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA BUKOBA**

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb. Na. AB.72/174/01C/170** **22 Julai, 2026**

Kuh: **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KIJANA WA KUJITOLEA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba, anawaalika Watanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi ya mkataba katika nafasi zifuatazo:-

## 1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU – AFYA – Nafasi 3

**Sifa za mwombaji:**

Awe mwenye elimu ya kidato cha IV au VI na Stashahada/Shahada katika fani ya Utunzaji Kumbukumbu za Afya kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi na Majukumu:**

i. Kupokea wagonjwa na kuwasajili kwenye vitabu vya mapokezi
ii. Kuwafungulia wagonjwa majalada
iii. Kutunza majalada ya wagonjwa na kumbukumbu zinazohusu wagonjwa.
iv. Kukusanya, kutunza, kuchambua na kutafsiri taarifa za Afya na zile zinazohusiana na Afya.
v. Kuandaa taarifa za Afya za Hospitali na kuziingiza kwenye mfumo wa taarifa.
vi. Kuhakiki/kusimamia ubora wa takwimu za wagonjwa.
vii. Kuandaa taarifa zote za Afya zinazohitajika katika ngazi ya Hospitali, Wizara n.k. na kuziwasilisha kwa Mganga Mfawidhi.
viii. Kusimamia utendaji wa kazi watumishi waliochini yako,
ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## 2. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI II - NAFASI 7

**Sifa za mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na Stashahada (Diploma) ya Uuguzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kutoa huduma za Uuguzi kwa wagomjwa
(ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya
(iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
(iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**3. MHANDISI UJENZI – NAFASI 1**

**Sifa za mwombaji:**

Awe mwenye elimu ya kidato cha IV au VI na Shahada (Degree) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi na Majukumu:**

i. Kufanya upimaji (survey) wa barabara, majengo na mifereji kama atakavyoelekezwa.
ii. Kusimamia ujenzi wa miradi barabara na majengo unaofanywa na wakandarasi wadogo wadogo.
iii. Kusimamia mafundi wa vikosi kazi vinavyo karabati nyumba za Hospitali na barabara.
iv. Kufanya makisio ya gharama na vifaa vya miradi midogo midogo.
v. Kufanya ukaguzi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali na barabara.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**4. DEREVA II NAFASI 3**

**Sifa za mwombaji:**

- Awe mwenye cheti cha kidato cha IV au VI na leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajari.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari yanayotolewa na Chuo cha Ufundi Stadi VETA au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**Majukumu:**

i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii) Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari
iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
vi) Kufanya usafi wa gari
vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MASHARTI YA KAZI;**

I. Ajira itakuwa ni ya kujitolea ya mwaka mmoja

II. Baada ya kipindi cha mkataba kuisha, Mfanyakazi atakayekuwa ameonesha ufanisi katika utendaji mkataba wake utaweza kuhuishwa.

**Mambo ya kuzingatia kwa waombaji**

I. Awe Mmiliki halali wa vyeti vya kitaaluma,

II. Awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Umma,

III. Awe na,

IV. Awe na utayari wa kujitolea katika eneo husika,

V. Awe hajawahi kuhukumiwa na Mahakama kwa makosa ya jinai au nidhamu,

VI. Awe na mwenendo na tabia njema inayokubalika na jamii, na

VII. Awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.

***Barua zote za maombi ziambatishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA, vyeti vya elimu na ujuzi, Maelezo binafsi (CV) yaliyoambatana na wadhamini wawili, leseni hai, barua ya Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Serikali za Mitaa pamoja na picha moja (1) ya rangi (Passport size).***

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA**

Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba,
S.L.P 265,
**BUKOBA.**

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE: 01/08/2026 SAA 8:00 MCHANA.**

Dkt. Museleta Nyakiroto
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA, BUKOBA**